# TAALUMA YA ISIMUJAMII KWA VYUO VIKUU

*Taaluma ya Isimujamii kwa Vyuo Vikuu* ni kitabu ambacho kimeandikwa hususan kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wa vyuo vikuu, wahadhiri, watafiti, wapenzi wasomaji wa kazi za Isimujamii hasa kwa lugha ya Kiswahili. Kazi hii ni ya kipekee kwa sababu inaangazia mkabala wa Kiislamu katika mambo ya Isimujamii kupitia marejeo ya aya za Qur'an na hadithi. Ndani ya kitabu hiki masuala nyeti yameakisiwa na yakachambuliwa kwa mifano halisi ya kijamii. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyoshughulikiwa ikiwa ni pamoja na uhusiano wa lugha na athari zake kwa jamii, nadharia za kijamii, lahaja, mawasiliano mapana, mchango wa Isimujamii katika elimu, upangaji na mabadiliko ya sera ya lugha. Aidha, kila sura ikihitimishwa kwa maswali ya kuchochea tafakuri, utafiti na utatuzi wa matatizo.



**Rukiya Harith Swaleh (PhD)** ni mhadhiri mwandamizi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Pwani, idara ya Lugha, Isimu na Fasihi. Ni mtaalamu katika Isimu na ushairi wa kale na amechapisha kazi kadhaa katika majarida kama Jahazi, Jakiiki, Twaweza, Ruwaza Afrika na mengineyo. Amewahi kusomesha katika shule ya upili, kufanya kazi katika Makavazi ya Kitaifa ya Kenya mjini Mombasa na sasa Chuo Kikuu cha Pwani.



**Dkt. Abdulrahim Hussein Taib Ali** ni mhadhiri mwandamizi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Pwani, na mtaalamu katika nyanja za isimujamii, fasihi ya Kiswahili na Uislamu. Amechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza Mkabala wa Kiislamu kama nadharia mbadala ya uhakiki wa kazi za fasihi na isimujamii. Amewahi kufundisha katika vyuo vikuu vya Egerton (Kenya), SUZA (Zanzibar), na Sebha (Libya), na ni mshiriki hai wa makongamano ya Kiswahili kitaifa na kimataifa. Machapisho yake yameonekana katika majarida ya Kioo cha Lugha, Jahazi, Mulika, IJAR, na mengineyo.

9 789912 985858